

Mambo 4 Muhimu Ambayo Wazazi Wanahitaji Kujua Kuhusu Ugonjwa wa Surua

Surua ni ugonjwa wa kuambukiza sana na unaweza kuwa hatari. Mtoto ambaye hajachanjwa anaweza kuugua ugonjwa wa surua anaposafiri kwenda ng'ambo au hata Marekani. Dozi mbili za chanjo ya MMR inatoa kinga dhidi ya ugonjwa wa surua katika mtoto wako.

Kama mzazi, huenda unashindwa kile unahitaji kujua kuhusu ugonjwa wa surua. CDC imeweka pamoja orodha ya ukweli muhimu zaidi kuhusu ugonjwa wa surua kwa wazazi kama wewe.



1. Ugonjwa wa surua unaweza kuwa hatari sana.

Watu wengine hudhania kwamba ugonjwa wa surua ni upele na joto kidogo tu ambayo inaisha baada ya siku chache lakini **ugonjwa wa surua unaweza kusababisha hali mbaya za kiafya**, hasa katika watoto walio na umri wa chini ya miaka 5. Hakuna njia ya kueleza mapema ukali wa dalili ambazo mtoto wako atapata.

- Tariban mtu 1 kati ya 5 huko Marekani ambao wanaugua ugonjwa wa surua watalazwa hospitalini
- Mtu 1 kati ya kila watu 1000 walio na ugonjwa wa surua wataapata uvimbe wa akili, ambao unaweza kupelekea uharibifu wa akili
- Mtu 1 hadi 3 kati ya 1000 walio na ugonjwa wa surua watakufa, hata wakiwa na huduma bora ya matibabu

Baadhi ya dalili za kawaida zaidi za ugonjwa wa surua zinajumuisha:

- joto kali (inaweza kupanda hadi zaidi ya 104° F),
- kikohozi,
- mafua (coryza),
- macho mekundu, yenye majimaji ([conjunctivitis \(uvimbe wa mboni ya jicho\)](#)), na
- upele (siku 3 hadi 5 baada ya dalili kuanza).

bit.ly/MeaslesSymptoms

2. Ugonjwa wa surua unaambukiza sana.

Ugonjwa wa surua huenea kwa njia ya hewa mtu aliyeambukizwa anapokohoa au kupiga chafya. Ni ugonjwa wenye kuambukiza sana kwamba ikiwa mtu mmoja anao, hadi watu 9 kati ya 10 walio karibu naye wataambukizwa ikiwa hawana kinga. Mtoto wako anaweza kuugua ugonjwa wa surua kwa kuwa tu katika chumba ambapo mtu aliye na ugonjwa wa surua yuko, hata hadi saa mbili baada ya mtu huyo kuondoka. Mtu aliyeambukizwa **anaweza kueneza ugonjwa wa surua kwa wengine hata kabla ya kujua kwamba anaugua ugonjwa huo**—kuanzia siku nne kabla ya kuwa na upele wa ugonjwa wa surua hadi siku nne baadaye.



bit.ly/MeaslesTransmission



3. Mtoto wako bado anaweza kuugua ugonjwa wa surua akiwa Marekani.

Ugonjwa wa surua ulitangazwa kukomeshwa Marekani miaka ya 2000 shukran kwa mpango wenye ufanisi wa kutoa chanjo. Kukomeshwa kunamaanisha kwamba ugonjwa huo haupo tena katika nchi hii. Hata hivyo, ugonjwa wa surua bado uko katika sehemu nyingi duniani.

Hata kama familia yako huwa haisafiri kwenda nchi za kimataifa, unaweza kuugua ugonjwa wa surua ukiwa mahali popote katika jamii yako. Kila mwaka, ugonjwa wa surua huletwa Marekani na wasafiri ambao hawajachanjwa (sanasana Waamerikani na wakati mwingine wageni wa nchi za nje) ambao huugua ugonjwa wa surua wanapokuwa katika nchi zingine. Mtu yeyote ambaye hana kinga dhidi ya ugonjwa wa surua yuko hatarini.

bit.ly/PlanForTravel



4. Una uwezo wa kulinda mtoto wako dhidi ya ugonjwa wa surua kwa kutumia chanjo salama na yenye ufanisi.

Kinga bora zaidi dhidi ya ugonjwa wa surua ni chanjo ya MMR (measles-mumps-rubella). Chanjo ya MMR hutoa kinga ya muda mrefu dhidi ya aina zote za ugonjwa wa surua.

Mtoto wako anahitaji dozi mbili za chanjo ya MMR kwa ajili ya kinga bora zaidi:

- Dozi ya kwanza katika umri wa miezi 12 hadi 15
- Dozi ya pili katika umri wa miaka 4 hadi 6

Ikiwa familia yako inasafiri kwenda ng'ambo, mapendekezo ya chanjo huwa tofauti kidogo:

- Ikiwa mtoto wako ana umri wa miezi 6 hadi 11, yeye anapaswa kupokea dozi 1 ya chanjo ya MMR kabla ya kusafiri.
- Ikiwa mtoto wako ana umri wa miezi 12 au zaidi, yeye atahitaji dozi 2 za chanjo ya MMR (iliyotenganishwa kwa angalau siku 28) kabla ya kuondoka.

Chanjo nyingine, chanjo ya MMRV (measles-mumps-rubella-varicella), ambayo inatoa kinga dhidi ya magonjwa 4, inapatikana pia kwa watoto walio na umri wa miezi 12 hadi miaka 12.

bit.ly/MealesVax